# TANZANIA LAND ALLIANCE (TALA)

# MAREKEBISHO YA SERA YA TAIFA YA ARDHI YA MWAKA 2016: Ni kwa maslahi ya nani?



UCHAMBUZI NA MAPENDEKEZO YA MTANDAO WA ASASI ZA UTETEZI WA HAKI ZA ARDHI (TALA)

# Yaliyomo ndani

VIFUPISHO VYA MANENO NA MAANA ZAKE ii

**SURA YA KWANZA 2**

1.1 UTANGULIZI 2

1.2 USULI 3

1.3 Masuala ya kuzingatiwa katika Marekebisho ya Sera ya Taifa ya Ardhi, 1995 4

**SURA YA PILI 8**

2.1 DOSARI ZA MCHAKATO WA MAREKEBISHO YA SERA 8

2.2 Tofauti za Kimchakato baina ya Sera ya Ardhi ya 1995 Mapitio ya Sera 2016 8

2.3 Miongozo na Sera za Kikanda katika Mapitio ya Sera ya Ardhi 9

2.4 Matumizi ya Takwimu za Ardhi katika Mapitio ya Sera 10

2.5 Kutokutanabahisha Msingi na Gurudumu la Maendeleo 11

**SURA YA TATU 15**

3.1 MAREKEBISHO YA SERA YA TAIFA YA ARDHI KATIKA MUKTADHA WA SASA 15

3.2 Umuhimu wa Mapitio ya Sera ya Taifa ya Ardhi 16

**SURA YA NNE 19**

UCHAMBUZI WA KIMAUDHUI WA RASIMU YA SERA YA TAIFA YA ARDHI 2016 19

4.1 UTAWALA NA USIMAMIZI WA ARDHI 19

4.2 MFUMO WA MILKI YA ARDHI 21

4.3 MFUMO WA UTATUZI MIGOGORO YA ARDHI 24

4.4 MILKI YA HATIMA YA ARDHI 26

4.5 USAWA WA HAKI ZA ARDHI KIJINSIA 28

4.6 UFUATILIAJI NA TATHMINI YA SERA YA ARDHI 30

**SURA YA TANO 33**

5.0 HITIMISHO 33

## VIFUPISHO VYA MANENO NA MAANA ZAKE

| | |
|---|---|
| **TALA** | Tanzania Land Alliance |
| **MKURABITA** | Mkakati wa Kurasimisha Rasilimali na Biashara Tanzania |
| **RS** | Regional Secretariat |
| **LGAs** | Local Government Authorities |
| **WMAs** | Wildlife Managament Areas |
| **SAGCOT** | Southern Agricultural Growth Corridor of Tanzania |
| **NFYDP** | National Five Years Development Plan |
| **NBS** | National Bureau of Statics |
| **MNRT** | Ministry of Natural Resources and Tourism |





# 1
# SURA

# SURA YA KWANZA

## 1.1 UTANGULIZI

Mtandao wa Mashirika yanayojihusisha na Utetezi wa Rasilimali Ardhi (TALA) pamoja na wadau wengine walikutana Jijini Dar es Salaam kufanya uchambuzi wa Rasimu ya Mapitio ya Sera ya Taifa ya Ardhi 2016. Katika kuipitia na kufanya uchambuzi wadau walibaini masuala kadha wa kadha ambayo Sera imeyajadili kwa kina na hayahitaji marekebisho, masuala ambayo Rasimu imeyajadili kwa ufinyu na yanahitaji kuboreshwa na masuala ambayo hayajaguswa kabisa na Rasimu ambayo yanahitaji kuwa sehemu ya rasimu ili kulinda haki na maslahi ya wazalishaji wadogo wadogo katika kupata, kutumia, kumiliki na utatuzi wa migogoro ya ardhi. Aidha uchambuzi unatoa tafsiri ya athari, kama vipengele hivyo vya kisera vitapitishwa kama vilivyo, pamoja na mapendekezo ya nini kifanyike.

Chapisho hili ni muhtasari wa uchambuzi huo wa kina. Shabaha yake kuu ni kuelimisha, na kusaidia kutoa mwongozo wa mjadala wa kitaifa, unaozingatia ushirikishwaji na maslahi mapana ya wazalishaji wadogo, kuhusu ardhi kwa ujumla na sera ya ardhi inayopendekezwa. Chapisho hili limegawanyika katika sura kuu tano, ambazo ni; Sura ya kwanza imebeba utangulizi na usuli wa mapitio ya Sera ya Taifa ya Ardhi mwaka 2016; Sura ya pili inahusu dosari za kimchakato katika mapitio ya Sera ya Taifa ya Ardhi mwaka 2016; Sura ya tatu inahusu marekebisho ya Sera ya Taifa ya Ardhi katika muktadha wa sasa; Sura ya nne inahusu uchambuzi wa kimaudhui wa Rasimu ya Sera ya Taifa ya Ardhi mwaka 2016 na sura ya tano ni hitimisho.



## 1.2 USULI

Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi iko katika mchakato wa kupitia na kurekebisha Sera ya Ardhi ya 1995. Mpaka kufikia mwezi Novemba 2016 wizara ilikuwa imetoa rasimu ya mswaada wa marekebisho ya Sera ya Ardhi ya 1995. Aidha, Wizara kupitia timu ya wataalamu, iliendelea kukusanya na kupokea maoni na ushauri toka kwa wadau mbalimbali juu ya maudhui na mapendekezo ya marekebisho katika sera. Ikiwa rasimu hii ya sera itapitishwa, ni dhahiri kuwa itaathiri sheria za ardhi na sheria za kisekta zinazohusiana na matumizi, usimamizi na utawala wa rasilimali ardhi.

Kupitia rasimu hii, Wizara inakiri wazi kwamba kadri ya maoni ya walio wengi waliohojiwa wakati wa mchakato wa ukusanyaji maoni ya wadau; Sera ya Ardhi ya 1995 ni nzuri isipokuwa kumekuwa na mapungufu ya kiutekelezaji, mfumo mbovu wa kiutawala katika ardhi, kutokuwepo kwa mpango kazi katika kusimamia utekelezaji, uwepo wa vyombo vingi katika usimamizi na utawala wa ardhi na kukosekana kwa utashi wa kisiasa.

Kwa mujibu wa Wizara hakuna tofauti kubwa baina ya Sera ya Ardhi ya 1995 na rasimu ya 2016 isipokuwa ubora wa rasimu ya sera ya ardhi 2016 ni kutokana na mchakato wa upatikanaji wa Sera hii kufuata miongozo ya Baraza la Mawaziri katika uandaaji wa sera unaozingatia mipango na mikakati ya maendeleo ya kitaifa; Mchakato wa marekebisho ya Sera ulifanyika Kikanda; Kuepukwa kwa makosa ya awali ya kiutekelezaji na Sera ya 2016 imeandaliwa kwa pamoja na mkakati wake wa utekelezaji. Kwa maoni ya Wizara, hii itasaidia kuepuka makosa yaliyojitokeza wakati wa utekelezaji wa Sera ya Ardhi ya 1995.

## 1.3 Masuala ya kuzingatiwa katika Marekebisho ya Sera ya Taifa ya Ardhi, 1995

Ni wazi kuwa kuna haja ya kufanya marekebisho katika Sera ya Ardhi ya 1995 lakini marekebisho haya yalihitaji kuzingatia hali ilivyo kwa sasa katika sekta ya ardhi. Masuala muhimu ya kuzingatia ni pamoja na haya yafuatayo:

(i) Sera na Sheria za Ardhi za sasa zimeshindwa kulinda haki za ardhi za watumiaji wadogo, kupitia matumizi ya mamlaka ya milki ya hatima uporaji umeongezeka kwa kiasi kikubwa katika kipindi cha miaka 20 ya utekelezaji wa Sera ya Ardhi ya 1995. Ardhi ya watumiaji wadogo, wakulima, wafugaji, warina asali na wavuvi imeendelea kutwaliwa kupisha ama miradi mikubwa ya uwekezaji katika kilimo, uchimbaji wa madini na vito, hifadhi za wanyama na mapori; au ulimbikizaji binafsi wa ardhi kwa ajili ya kuikodisha kwa watu wengine, au kusubiri bei ya ardhi kupanda na kuiuza kwa faida. Uporaji wa aina hii mara nyingi umetokea bila ushirikishwaji wa jamii katika maeneo husika.

(ii) Ongezeko la migogoro baina ya watumiaji ardhi kama vile baina ya wakulima na wafugaji, wanavijiji na wawekezaji, migogoro ya mipaka ya vijiji na migogoro baina ya vijiji na hifadhi mbalimbali.

(iii) Upanukaji holela wa miji na ama uanzishwaji wa mamlaka za miji usiozingatia maslahi ya watumiaji wa ardhi hasa wakulima na wafugaji. Upanukaji huu holela umepelekea upotevu wa mali na maisha ya watu na hasara za kifedha na kuweka rehani amani, utulivu na utengamano miongoni mwa jamii

(iv) Sera ya uchumi ya serikali ya awamu ya tano ni uchumi wa viwanda. Ili sera hii ifanikiwe haina budi kuongozwa na dhana ya maendeleo inayotambua uhusiano unaotegemeana kati ya kilimo na viwanda ambapo viwanda vitatumia malighafi zitokanazo na kilimo na hivyo kuwa soko endelevu la mazao ya wakulima. Aidha viwanda vitatengeneza bidhaa mbalimbali kwa ajili ya wakulima, kama vile pembejeo za kilimo na bidhaa zingine za matumizi ya kawaida. Kwa maana hiyo wakulima watakuwa soko la bidhaa zizalishwazo na viwanda. Ili kutimiza azma hii Sera ya ardhi lazima itambue na kulinda haki za ardhi za wazalishaji wadogo ambao ndio wengi, na kuweka miundo mbinu ya kisasa vijijini kama vile umeme na barabara ili kupafanya vijijini mahala pa uzalishaji wa kilimo na viwanda.

Yote haya yanahitaji kuunganishwa kwa pamoja na dira ya uchumi wa kitaifa ambayo msingi wake mkuu ni kundi la wazalishaji wadogo vijijini, ambao kati yao watazalisha ziada na kukuza mitaji yao na kuiwekeza katika maeneo mengine ya uzalishaji, kama vile viwanda vidogo vidogo vya kuchakata mazao ya kilimo pale pale kijijini, na wanaweza kujitanua na kuwekeza katika maeneo mengine kwa kuanzisha viwanda vikubwa zaidi. Msingi wa aina hii ya uchumi unaohusisha kilimo na viwanda ni ukuaji wa maendeleo na mabadiliko ya kiuchumi na kijamii ambapo chanzo kikubwa cha mtaji na mabadiliko (transformation) ni kutokana na uzalishaji wa ndani.

Kwa vile mchakato wa marekebisho ya Sera ya ardhi umefikia hatua ya kutoa rasimu, na kwa vile katika hatua zote za awali mpaka kufikia kutoa rasimu ya sera kumejitokeza dosari mbali mbali juu ya ushirikishwaji wa wananchi na wadau wengine usioridhisha, Asasi za kiraia zinazojihusisha na masuala ya utetezi

na ushawishi juu ya haki za ardhi kwa makundi mbalimbali ya watumiaji wa ardhi yaliamua kukutana na kujadili namna nzuri ya kupanua ushiriki wa wananchi na wadau wengine katika kujadili na kutoa maoni yao juu ya rasimu ya sera ya ardhi inayopendekezwa.





# SURA 2

# SURA YA PILI

## 2.1 DOSARI ZA MCHAKATO WA MAREKEBISHO YA SERA

Mchakato wa marekebisho ya Sera ya Ardhi ya 2016 umekuwa na dosari zifuatazo.

(i) Umefanyika kikanda, kwa kuzingatia mgawanyo wa kanda za kiutawala za usimamizi wa ardhi, ukihusisha sampuli yenye kutiliwa shaka ikizingatiwa idadi ya washiriki na maeneo walikotoka.

(ii) Mchakato unaacha kwa kiasi kikubwa tashwishwi ya kwamba msukumo wa mabadiliko haya sio madai halisi ya makundi ya wazalishaji wadogo bali mwendelezo wa shinikizo la siku nyingi wa kundi linalotaka kuona ardhi inabinafsishwa.

(iii) Kwa msukumo wa kundi hili na maslahi yake haikuonekana haja ya kushirikisha makundi ya wazalishaji hususan wakulima vijijini, wavuvi, warina asali, wafugaji na waokota matunda ambao tegemeo lao kubwa ni rasilimali ardhi katika kuendesha maisha yao.

## 2.2 Tofauti za Kimchakato baina ya Sera ya Ardhi ya 1995 Mapitio ya Sera 2016

Kuna tofauti kadha wa kadha za kimchakato katika upatikanaji wa Sera ya Taifa ya Ardhi mwaka 1995 na mapitio ya Sera mwaka 2016, tofauti hizi ni kama zifuatazo;

(i) Mchakato wa upatikanaji wa Sera ya Ardhi ya 1995 ulitanguliwa na Utafiti na Ripoti ya Tume ya Rais ya Uchunguzi wa Masuala ya Ardhi, iliyofuatiwa na mjadala wa muda mrefu uliodumu kwa takribani miaka mitatu (1995 – 1999), kabla ya kupitishwa kwa Sheria za Ardhi mwaka 1999,

(ii) Mchakato wa kupitia na kurekebisha Sera ya Ardhi wa mwaka 2016 umefanyika kwa muda mfupi, kwa ukimya na pasipo kushirikisha watu wengi. Kiasi cha watu 705 walioainishwa kama wanavijiji ndio walishiriki katika kutoa maoni, na watu 765 wasio wanakijiji walishiriki.

(iii) Katika Tanzania idadi ya wazalishaji wadogo ni 65.5% iweje ushiriki wao katika mchakato huu uwe mdogo hivyo na kuzidiwa na kundi lisilo la wazalishaji. Maoni mengi yaliyokwishatolewa hayakuzingatiwa hata katika fursa kidogo zilizotolewa.

## 2.3 Miongozo na Sera za Kikanda katika Mapitio ya Sera ya Ardhi

Rasimu inataja kuwa imezingatia miongozo ya Kisera ya Umoja wa Afrika juu ya Uandaaji na Utekelezaji wa sera ya ardhi pamoja na miongozo mingine ya Kimataifa na kikanda, uchambuzi unadhihirisha wazi kuwa miongozo hii imetajwa tu bila ya maudhui yake kuzingatiwa. Miongozo hii katika ujumla wake inatanabahisha wazi hatua mbalimbali za kuzingatiwa katika uandaaji wa sera ya ardhi na hatimaye utekelezaji wake, miongoni mwa hatua hizi ni pamoja na;

- Uwazi katika mchakato wa upatikanaji wa Sera ya ardhi
- Ushirikishwaji wa wadau, ikiwamo watumiaji wa ardhi, asasi za kiraia na makundi mengineyo yenye maslahi katika ardhi

Malengo ya Maendeleo Endelevu (Sustainable Development Goals) ya Umoja wa Mataifa yanazitaka nchi wanachama wa Umoja wa Mataifa kuhakikisha kuwa kufikia 2030 zinaongeza

uzalishaji katika kilimo na kipato kwa makundi ya wazalishaji wadogo, hususani wanawake, wenyeji asilia, wakulima wadogo, wafugaji na wavuvi. Kwa mujibu wa malengo haya ya Umoja wa Mataifa mambo ya kuzingatiwa ili shabaha hizi zifikiwe ni pamoja na kuwepo;

- Usawa katika upatikanaji wa rasilimali ardhi;
- Rasilimali za uzalishaji, ujuzi, huduma za kifedha, masoko na fursa nyinginezo.

Rasimu ya Sera ya Ardhi inataja uhakika wa milki na upatikanaji sawa wa ardhi kwa ujumla bila kuzingatia kuwa miaka nenda miaka rudi hili limekuwa kilio kikubwa kwa makundi ya wazalishaji wadogo. Ardhi imeendelea kutwaliwa bila kuzingatia maslahi ya makundi haya, hasa wakazi katika ukanda wa pwani, hifadhi za taifa, na maeneo yaliyoainishwa kama ya uwekezaji. Makundi haya yameendelea kuondolewa, mara nyingine kimabavu, ili kupisha wenye uwezo kifedha na mamlaka za ndani na nje kutumia rasilimali ardhi na rasilimali nyinginezo zinazopatikana katika maeneo husika.

## 2.4 Matumizi ya Takwimu za Ardhi katika Mapitio ya Sera

Kwa upande mwingine rasimu ya Sera ya Ardhi inatoa takwimu zenye walakini zinazoweza kushawishi kuwa kuna ardhi kubwa kwa ajili ya shughuli za uzalishaji zisizokuwa na athari kwa wazalishaji wadogo. Mfano ni pale Rasimu ya Sera inapobainisha kuwa eneo la ardhi ya hifadhi limeendelea kubakia kuwa ni asilimia 28 wakati eneo hilo limeendelea kuongezeka. Kadri ya vyanzo rasmi tofauti, mathalani Wizara ya Mali Asili na Utalii na Ofisi ya Takwimu, eneo la hifadhi limeendelea kuongezeka na kufikia asilimia 40 ya ardhi yote nchini, kama inavyoonyeshwa katika kielelezo hapo chini;

| Na | AINA YA ARDHI YA HIFADHI | UKUBWA WA ARDHI (km$^2$) | IDADI KUNDI HUSIKA | ASILIMIA YA ARDHI YOTE |
|---|---|---|---|---|
| 1 | Hifadhi za Taifa | 57,415 | 16 | 6% |
| 2 | Mamlaka za Hifadhi (Conservation Areas) | 8,292 | 1 | 1% |
| 3 | Hifadhi za Misitu | 32133.89 | 33 | 3% |
| 4 | Mapori ya Akiba | 117,755.40 | 28 | 12% |
| 5 | Maeneo ya Ramsar (Ramsar Sites) | 48,684 | 4 | 5% |
| 6 | Hifadhi za Jamii za Wanyamapori (WMAs) | 29,518.4 | 38 | 3% |
| 7 | Mapori Tengefu (Game Controlled Areas) | 58,565.02 | 44 | 6% |
| 8 | Hifadhi za Bahari (Marine Parks) | 1,380 | 8 | 4% |
| | **JUMLA** | | | **40%** |

**Chanzo:** NBS 2015; Environmental Statistics 2014 & MNRT 2013; Wildlife Sub-Sector Statistical Bulletin, 2013 Edition

## 2.5 Kutokutanabahisha Msingi na Gurudumu la Maendeleo

Rasimu iko kimya katika kubainisha nani au kundi gani na ni rasilimali zipi ni msingi wa maendeleo. Ili kukuza na kuchochea uzalishaji katika kilimo rasimu; inasisitiza urasimishaji wa ardhi kama mojawapo ya nyenzo ya kuwawezesha wamilki watumie ardhi zao kama rehani kupatia mikopo ya kibenki; imetanabahisha wazi wazo la kutoza kodi kama chachu ya kuwafanya wenye maeneo waweze kuyaendeleza na kwa mara ya kwanza hii itahusisha ardhi za vijiji; kwa mujibu wa rasimu uendelezwaji

hafifu wa ardhi za vijiji unatokana na sababu kwamba wanavijiji hawalipii ushuru wa ardhi na hivyo basi kutokuona umuhimu wa ardhi.

Hii ni dhana potofu na inaendana na dhana iliyojengeka kwa muda mrefu kwamba wazalishaji wadogo ni kikwazo cha maendeleo. Njia mojawapo ni kuwawezesha wakulima wakubwa hasa wawekezaji kuweza kupata ardhi kwa urahisi kwa misingi ya kwamba ndio wenye uwezo na ujuzi wa kuyaendeleza maeneo yao kwa faida. Kwa kutokuzingatia tatizo la msingi lilipo utekelezaji wa kipengele hiki utaishia kwenye uporaji na unyang'anyi wa ardhi za vijiji, uendelezaji wa ardhi vijijini utawezekana tu pale ambapo masuala yafuatayo yatazingatiwa:

- Serikali itaweka kipaumbele kwenye sekta ya Kilimo kwa kuwawezesha wazalishaji wadogo kutumia ardhi zao kwa uzalishaji zaidi. Tanzania bado kwa sehemu kubwa msingi wake ni wazalishaji wadogo ambapo takribani asilimia 70 wanategemea ardhi moja kwa moja kuendeleza maisha yao. Uwekezaji kwa kundi hili utachochea uzalishaji zaidi na uwepo wa viwanda vya kuongeza thamani, utachangia kukua kwa soko la ndani, na kuchochea ukuaji wa viwanda vya kati na vikubwa hivyo basi kufikia ndoto ya Tanzania ya viwanda na iliyo katika hadhi ya uchumi wa kati kufikia 2025
- Maendeleo ya viwanda yatawezekana pale ambapo dhana ya kuhimiza maendeleo vijijini itafanikiwa. Matokeo ya utafiti wa Tume ya Rais ya Uchunguzi wa Masuala ya Ardhi yalibainisha wazi kuwa upo uwezekano wa kutengeneza na kulimbikiza mtaji wa ndani kutokana na wazalishaji wadogo wadogo ikiwa tu watatambuliwa kuwa ndio msingi wa maendeleo. Tofauti kati ya ulimbikizaji wa aina hii na ule unaotegemea uwekezaji toka nje ni kwamba ulimbikizaji huu unakuwa ndio msingi wa ujenzi wa uchumi wa kitaifa unaotegemea kwa sehemu kubwa uendelezaji na ujenzi wa misingi ya uzalishaji mali wa ndani. Ndio msingi wa Tume kupendekeza kuwa pamoja na kuwa na ukomo wa ardhi katika umilki wa ardhi vijijini wa ekari 200, mwanakijiji mwenye uwezo wa kuendeleza zaidi ya hapo apatiwe ardhi katika kundi la ardhi ya Jumla, ama iliyotengwa kwa malengo ya uwekezaji.



SURA

3

# SURA YA TATU

## 3.1 MAREKEBISHO YA SERA YA TAIFA YA ARDHI KATIKA MUKTADHA WA SASA

Rasimu ya Sera imeeleza wazi kuwa imezingatia miongozo ya kitaifa ya mipango ya maendeleo, mwongozo mojawapo ni Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano (NFYDP 2016/2017-2020/2021). Katika eneo la ardhi mpango huu unaeleza bayana kwamba:

(i) Sera ya Ardhi 1995 na Sheria za Ardhi Namba 4 na Sheria ya Ardhi ya Vijiji Namba 5, kwa namna zilivyo hivi sasa, hazikidhi mahitaji ya kuwezesha maendeleo ya viwanda;

(ii) Urasimishaji na Ubidhaifishaji wa ardhi kwa pamoja waweza kuwa nyenzo nzuri katika utatuzi wa migogoro ya ardhi, ikiwemo migogoro baina ya wawekezaji na wamiliki wa ardhi, na watumiaji wengineo wa ardhi

(iii) Utwaaji wa ardhi kwa ajili ya uwekezaji limekuwa ni zoezi gumu lenye kupitia taratibu ndefu zenye kuchosha

(iv) Urasimu na taratibu hizo umeongeza gharama kwa mwekezaji na hivyo kuwa kikwazo katika kuvutia uwekezaji

Kwa sababu hizi Mpango unaeleza haja ya msingi ya kufanya marekebisho kwa Sera ya Ardhi 1995 na Sheria zake ili kuondoa migongano na sheria nyinginezo ili kuwezesha yafuatayo:

(i) Kuwezesha ardhi iliyopimwa kuwa chanzo endelevu cha mapato ya serikali, lakini muhimu zaidi ardhi kuwa kivutio cha uwekezaji, mtaji na pia dhamana ya mikopo kwa taasis za fedha. Hii itajumuisha urasimishaji wa makazi holela mijini na

kuongeza namba ya vijiji vilivyopimwa na idadi ya wanavijiji wenye hati milki za kimila (CCROs). Hivyo basi kuna haja ya kuimarisha mpango wa MKURABITA na utekelezaji wake.

(ii) Uanzishwaji wa Kituo kimoja (One-Stop Centre) cha masuala ya ardhi ili kuwezesha wawekezaji wanaohitaji ardhi kubwa kupitia hapo; na kwa mikoani na wilayani kutakuwa na vituo vya rufaa kwa wawekezaji wanaohitaji ama katika Sekretariati za Mikoa (RS) au Mamlaka za Serikali za Mitaa (LGAs)

(iii) Katika ngazi ya Taifa na Serikali za Mitaa kutakuwepo na benki ya ardhi maalum kwa ajili ya shughuli za viwanda (zikiwa na huduma zote muhimu kama; hati, miundo mbinu ya barabara na umeme, skimu za umwagiliaji n.k.)

(iv) Kupanua na kuboresha Mfuko wa Ulipaji Fidia ya Ardhi (Land Compensation Fund), kuwezesha ulipaji fidia kwa wakati kwa maeneo yaliyotengwa ama kuainishwa kwa malengo ya uwekezaji

Ni wazi kuwa Mpango wa Maendelo wa Miaka Mitano unaifanya ardhi kuwa chanzo cha mapato, na katika mipango hii ni wazi kuwa nafasi ya mzalishaji mdogo haipo. Hii yawezekana kuwa sababu mojawapo kwa nini rasimu haitaji wazi ni nani mlengwa na mnufaika wa marekebisho haya.

## 3.2 Umuhimu wa Mapitio ya Sera ya Taifa ya Ardhi

Upitiaji upya wa Sera ya Ardhi ya 1995 na kuifanyia marekebisho iwe ni fursa adhimu ya kuanzisha mjadala wa kitaifa ili kuona kwa mapana na marefu njia na shabaha ya maendeleo tunayoitaka na nafasi ya wazalishaji wadogo na ardhi katika kufikia shabaha hizo.

Aidha, ni muhimu wakati wote kuzingatia haja ya kujenga miundombinu vijijini ili kuviwezesha vijiji kuwa ni vitovu vya maendeleo ya viwanda na uzalishaji nchini kupitia yafuatayo:

(i) Suala la uanzishwaji na uimarishaji wa ushirika katika ngazi za msingi, uwezeshaji kwa maana ya serikali kurejea na kuchukua hatamu katika kuwawezesha kimitaji wazalishaji wadogo na pia kuboresha huduma za ugani vijijini kwa wakulima wadogo.

(ii) Inafahamika wazi kuwa Tanzania kwa mfano ni nchi ya tatu kwa wingi wa mifugo Afrika, lakini ni kwa kiasi gani inafaidika na ufugaji huu? Na ni kwa jinsi gani serikali inajishughulisha na uendelezaji wa sekta ya mifugo ili kuhakikisha kuwa utajiri huu unatumika katika kuleta na kuchangia katika maendeleo ya viwanda! Kwa jinsi ilivyo sasa hakuna mahusiano ya moja kwa moja kati ya sekta ya mifugo na viwanda. Kuna haja ya kulitazama hili ili kujenga uhusiano wa maendeleo ya viwanda na ufugaji nchini. Kwa mtazamo huu wafugaji asilia ndio haswa msingi wa maendeleo na ukuaji wa sekta ya viwanda vinavyohusiana na mifugo.

(iii) Wafugaji, hasa wale wa asili, wanapitia changamoto za kila aina, hizi ni pamoja na jitihada za kuwabadili kwa mabavu ili waachane na aina yao ya ufugaji – yaani kinachoonekana kuwa ufugaji wa kijima; kutozingatiwa kwa chanzo hasa cha migogoro ya wafugaji na wakulima; na kusumbuliwa kwa wafugaji pale mifugo yao inapoonekana katika maeneo ya miji na lawama kuelekezwa kwao badala ya mipango na taratibu zisizofaa zinazoruhusu miji kukua na kupanuka kiholela na kuathiri shughuli za watumiaji wengine wa ardhi.




# SURA YA NNE

## UCHAMBUZI WA KIMAUDHUI WA RASIMU YA SERA YA TAIFA YA ARDHI 2016

### 4.1 UTAWALA NA USIMAMIZI WA ARDHI

Rasimu ya Sera ya Taifa ya Ardhi mwaka 2016 inaweka misingi inayohakikisha kwamba Kamishna wa Ardhi anabaki kuwa Mamlaka pekee ya usimamizi wa makundi yote ya ardhi nchini. Kuwepo kwa wataalamu wa ardhi katika ngazi ya wilaya na ngazi za chini.

**Muktadha:** Huu ni utaratibu ambao una lengo la kumwongezea zaidi Kamishna wa Ardhi mamlaka hasa kwenye ardhi ya kijiji kutoka mamlaka ya ushauri hadi kuwa na mamlaka pekee ya usimamizi wa ardhi ya kijiji. Hoja ya kuweka wataalamu wa ardhi mpaka ngazi za chini ni jambo jipya linaloletwa na Rasimu ya Sera ya Ardhi 2016.

**Maana ya Sera hii ni kuwa;**

(i) Mamlaka ya usimamizi wa ardhi zote nchini utakuwa chini ya Kamishna wa Ardhi hivyo kuondoa mamlaka ya serikali ya kijiji ya usimamizi wa ardhi ya kijiji,

(ii) Utaratibu wa Kamishna kuwa ndio mamlaka pekee ya usimamizi unapingana na dhana ya kushusha madaraka kwa wananchi na kulenga kulimbikiza madaraka ngazi za juu hivyo kunyima wanavijiji nafasi ya kufanya maamuzi kuhusu ardhi zao.

(iii) Utaratibu unaopendekezwa wa kuwepo kwa wataalamu wa ardhi hadi vijijini utaondoa mamlaka za serikali za kijiji na wananchi katika usimamizi na maamuzi kuhusu ardhi yao.

(iv) Utaratibu huu mpya unaongeza urasimu na mianya ya rushwa kwa watendaji ambao katika ngazi walipo wamekuwa chanzo cha upindishaji wa sheria na kutumia mamlaka yao kujinufaisha wao wenyewe.

### Hali halisi ya usimamizi wa ardhi ya vijiji tangu mwaka 1995 hadi 2016

(i) Sheria za ardhi zilimpa Kamishna wa ardhi kuwa na mamlaka ya ushauri kwenye serikali za vijiji na wanavijiji juu ya usimamizi wa ardhi ya kijiji.

(ii) Kumekuwepo na matumizi mabaya ya mamlaka hiyo hasa pale ushauri unaotoka kwa Kamishna kuchukuliwa kama ni uamuzi wa mwisho hivyo kuchukua nafasi ya maamuzi ya wanakijiji kuhusu ardhi yao.

(iii) Wakati mwingine wanavijiji wamekuwa wakikosa ushauri wanaohitaji kutoka kwa Kamishna na pale unapopatikana basi unatolewa kwa lengo la kufanikisha maombi ya ardhi yanayohusisha uhawilishaji kutoka ardhi ya Kijiji kuwa ya Jumla kwa ajili ya shughuli za uwekezaji.

(iv) Utaratibu ulioainishwa kisheria wa ardhi ya kijiji kusimamiwa na Serikali ya kijiji na maamuzi ya mwisho kufanywa na Mkutano Mkuu wa Kijiji. Utaratibu huu umefanya kazi vizuri hasa katika maeneo ambayo wanakijiji wana uelewa mzuri wa haki zao za kisheria na taratibu za ardhi. Badala ya kuimarisha uwezo na mamlaka ya wanavijiji kusimamia ardhi yao wenyewe Sera inayopendekezwa inakusudia kuipora haki hiyo na hivyo kumuongezea Mamlaka zaidi Kamishna juu ya usimamizi wa ardhi ya kijiji. Hii ni wazi itafanikisha zaidi uporaji wa ardhi za vijiji badala ya kuzilinda.



### Mapendekezo kuhusu Usimamizi wa Ardhi ya Kijiji

(i) Halmashauri za vijiji na Mikutano Mikuu wa Kijiji vitakuwa na dhamana juu ya ardhi ya kijiji husussan ugawaji na usimamizi wa matumizi.

(ii) Mkutano Mkuu wa kijiji kiwe ndio chombo chenye mamlaka ya juu (Milki ya hatma) katika maamuzi juu ya ardhi ya kijiji, na wananchi wapewe elimu zaidi juu ya mamlaka yao hii.

(iii) Serikali za vijiji zijengewe uwezo wa kusimamia ardhi na maliasili zilizopo ndani ya vijiji kwa niaba ya wanakijiji wote.

## 4.2 MFUMO WA MILKI YA ARDHI

Rasimu ya Sera ya Taifa ya Ardhi inatambua kuwa;

- Mfumo wa milki wa Hati za Kimila na kuainisha kuwa utakuwa na hadhi sawa kisheria,
- Mgawanyo wa ardhi katika makundi matatu ya Ardhi ya Kijiji, Hifadhi na Jumla,
- Ukomo wa ukubwa wa ardhi itakayotolewa kwa ajili ya uwekezaji uwe ni miaka 33 itakayoweza kurejewa,
- Haki kwa Wawekezaji kupewa Hati badala ya Hati hafifu pale ambapo wanahitaji kuendeleza maeneo kwa kujenga majengo ya umiliki wa pamoja.
- Kuanzishwa kwa kodi ya ardhi kwenye makundi yote na pia kutakuwa na kodi maalumu kwa ardhi ambazo hazijaendelezwa

**Muktadha:** Rasimu imeendeleza utaratibu uliokuwepo kwenye milki na kwenye makundi ya ardhi. Vile vile rasimu imeendelea kuainisha kuwepo kwa ukomo wa ukubwa wa ardhi inayotolewa kwa ajili ya uwekezaji. Mambo mapya yaliyoainishwa kwenye mfumo wa milki kwa mujibu wa Rasimu ni ukomo wa umiliki

wa ardhi wa miaka 33 kwa Wawekezaji pamoja na utozwaji wa kodi katika makundi yote ya ardhi na kodi maalumu kwa ardhi ambazo haziendelezwi.

### Maana ya Sera hii ni kuwa;

(i) Matamko ya kisera hayajaainisha wazi ukomo wa ukubwa wa ardhi unaopendekezwa kutolewa kwa wawekezaji hivyo hali ya kuendelea kuhodhi ardhi kubwa kupita mahitaji halisi itaendelea.

(ii) Wawekezaji wa kigeni watapewa hati ya umiliki wa ardhi watakayoiendeleza kwa ajili ya umiliki wa pamoja (Unit titles).

(iii) Pendekezo la utaratibu wa kutoza kodi kwa makundi yote ya ardhi utakuwa na athari kubwa kwa wamiliki wa ardhi ndani ya vijiji maana watakaposhindwa kulipa kodi hizo ardhi zao zitachukuliwa.

### Uhalisia wa Mfumo wa Milki ya Ardhi tangu mwaka 1995 hadi 2016

(i) Utaratibu uliowekwa na Sera ya Taifa ya Ardhi 1995 na Sheria za Ardhi 1999 ulitambua mifumo miwili ya umiliki wa ardhi (Miliki ya Hati na Miliki ya Kimila) na kuipa hadhi sawa kisheria. Pamoja na hadhi zote za miliki kulingana kisheria taasisi za kifedha zimekuwa zikikataa kupokea Hati za kimila kama dhamana ya mikopo na hivyo kuleta dhana kwamba hati hizo hazina hadhi sawa kisheria na ardhi inayomilikiwa kwa hati.

(ii) Hoja ya ukomo wa ukubwa wa ardhi ilibaki kama matamko tu na haijawahi kuwekewa kanuni au kiwango wala kutekelezwa wakati wowote ule.

(iii) Utaratibu wa wawekezaji kupatiwa hati hafifu za umiliki umekuwa ukikiukwa na wapo wawekezaji waliopatiwa hati yenye ukomo wa miaka 99 na baadhi yao kutelekeza mashamba hayo huku yakiwa na rehani au kuishia kuwakodishia wanavijiji.

(iv) Kumekuwepo na msukumo wa kuhakikisha kuwa wawekezaji wanapewa haki sawa na Watanzania katika umiliki wa ardhi nchini.

### Mapendekezo kuhusu Mfumo wa Milki ya Ardhi:

- Utaratibu wa kutoza kodi za ardhi ufanyike kwenye makundi mengine ya ardhi isipokuwa ardhi ya kijiji.
- Ukomo wa ukubwa wa umiliki wa ardhi ndani ya vijiji uwe ni Ekari 100, hii inazingatia mahitaji ya ardhi ndani ya kijiji na kuondoa uwezekano wa kuhodhi ardhi.
- Endapo mtu anamiliki ardhi zaidi ya kijiji kimoja ukomo wake utahesabiwa kwa kujumlisha ukubwa wa ardhi zote anazomiliki. Ikiwa mmiliki anahitaji eneo zaidi ya ekari 100 basi mtu huyo aombe ardhi kwenye kundi la ardhi ya jumla.

## 4.3 MFUMO WA UTATUZI MIGOGORO YA ARDHI

Rasimu ya Sera ya Taifa ya Ardhi inaazimia masuala yafuatayo kuhusu mfumo wa utatuzi wa migogoro ya ardhi nchini;

- Kufanya mabadiliko kwenye mfumo wa mabaraza kuanzia ngazi ya vijiji hadi wilaya,
- Kuanzisha Mabaraza ya Ardhi na Nyumba ya Wilaya katika kila wilaya nchini.

**Muktadha:** Sera na sheria zilizopo zimeweka mfumo wa utatuzi wa migogoro ya ardhi kuanzia ngazi ya kijiji unaoishirikisha jamii kwa kuteua wajumbe wa mabaraza ya ardhi kupitia halmashauri za vijiji na mikutano mikuu ya vijiji. Ngazi nyingine kwenye mfumo huo ni Mabaraza ya Kata, Mabaraza ya Ardhi na Nyumba ya Wilaya, Mahakama Kuu na Mahakama ya Rufani. Rasimu ya Sera ya Taifa ya Ardhi 2016 inapendekeza kuendeleza mfumo huo kwa kuufanyia maboresho.

### Maana ya Sera hii ni kuwa;

(i) Mfumo uliopo sasa wa utatuzi wa migogoro ya ardhi utaendelea kutumika bila kuainisha jinsi ya kukabiliana na mapungufu yaliyopo kama vile rushwa, uhaba wa vifaa, uelewa mdogo wa Watendaji katika vyombo husika, gharama kubwa za uendeshaji wa mashauri, na muda mrefu wa usikilizwaji wa mashauri kwenye mabaraza na mahakama.

(ii) Mfumo uliopo wa Mabaraza ukiendelea kutumika una athari hasi kwa haki za ardhi kwa kuwa hauna utaratibu wa uwajibikaji kwa kuwa unasimamiwa na mamlaka zaidi ya moja ambazo zina taratibu zinazotofautiana.

(iii) Rasimu haijaainisha ngazi nyingine za mfumo huo na wala haijaaanisha mapendekezo ya maboresho yanayokusudiwa.

### Uhalisia wa Mfumo wa Utatuzi wa Migogoro ya Ardhi tangu 1995 hadi 2016

(i) Mfumo huu unakabiliwa na changamoto nyingi zikiwemo kuingiliwa na mamlaka za kiutendaji kuanzia ngazi ya kijiji, Kata, na Wilaya, na wakati mwingine wanasiasa.

(ii) Matumizi ya mila na desturi za maeneo husika zinaonekana kutoendana na hali halisi ya mabadiliko ya kijamii na hivyo kutotenda haki iliyokusudiwa pale zinapotumiwa kulingana na maelekezo ya mfumo wa kisheria uliopo.

(iii) Mfumo hauna mtiririko unaoonyesha ngazi za uwajibikaji hivyo kuwa na athari kwenye utoaji wa haki na udhibiti wa maadili.

(iv) Mfumo wa Mabaraza hasa ya Wilaya hayapo nchi nzima hivyo kukosesha wananchi wengi nafasi ya kupata haki zao. Vile vile Mabaraza yaliyopo hayajawezeshwa kikamilifu ili yaweze kutoa haki kwa wakati na kuzingatia taratibu za kisheria.

(v) Mwaka 2013 Tume ya Mabadiliko ya Sheria (Law Reform Commission) ilifanya utafiti juu ya mfumo wa utatuzi wa migogoro na kupendekeza mabadiliko makubwa yakiwemo kuweka mfumo wote chini ya mhimili wa mahakama ila mpaka sasa hamna utekelezwaji wa mapendekezo hayo.

### Mapendekezo juu ya Mfumo wa Utatuzi wa Migogoro ya Ardhi

(i) Halmashauri za Wilaya zitoe mwongozo kwa mamlaka za vijiji kuhus taratibu za uanzishwaji wa mabaraza na uendeshaji wa mashauri katika Mabaraza ya ardhi ya vijiji kwa njia za usuluhishi ili kuepuka athari za tafsiri potofu ya matumizi ya mila kandamizi katika vijiji,

(ii) Mifumo ya asili ya utatuzi wa migogoro ya ardhi kwenye maeneo husika itambuliwe na kuimarishwa ili kuhakikisha inatekeleza majukumu yake bila kuvunja sheria za nchi,

(iii) Serikali ianzishe Mahakama zitakazokuwa zinahama katika ngazi ya Wilaya (Circuit Courts) ili ziweze kutatua mashauri ya ardhi kwenye maeneo husika pale ambapo usuluhishi utakuwa umeshindikana kwenye ngazi ya Baraza la Ardhi la Kijiji.

## 4.4 MILKI YA HATIMA YA ARDHI

Rasimu ya Sera inasema kuwa miliki ya hatima ya ardhi itabaki kwa Rais.

**Muktadha:** Huu ni utaratibu ambao ulitumika tangu kipindi cha ukoloni ili kuwasaidia wakoloni kupora ardhi ya wananchi. Sera ya Taifa ya Ardhi ya mwaka 1995 iliendeleza utaratibu huu. Miaka 20 tangu Sera kuanza kutumika nchini utaratibu huu unaendelea kutumika hata katika rasimu ya Sera ya Ardhi ya 2016.

### Maana ya Sera hii ni kuwa;

(i) Mwenye dhamana ya kumiliki ardhi yote ni Rais na wala si wananchi,

(ii) Rais ana mamlaka ya kutwaa, kuhawilisha, na kufuta hati ya ardhi ya mtu yeyote sehemu yeyote nchini na kwa ukubwa wowote anaoutaka kwa maslahi ya umma,

(iii) Chombo cha utendaji cha dola, hususan Wizara ya Ardhi na watendaji wake, ndiyo pekee watakuwa na uwezo wa kufanya maamuzi mazito ya ugawaji wa ardhi, na matumizi na maendeleo yake bila kushurutishwa na sheria, kushirikisha wananchi au vyombo vyao vya uwakilishi, kama vile Bunge na Mkutano Mkuu wa Kijiji na kupata idhini yao,

(iv) Dola kuhodhi milki ya hatima ya ardhi ni jambo linaloathiri kwa kiwango kikubwa demokrasia kwa ujumla na kupunguza uwazi katika utawala wa nchi na kutoa mwanya kwa wabadhirifu na wala-rushwa kuendeleza maovu yao kwa siri bila kuwajibika hadharani.

### Uhalisia wa Milki ya Hatma tangu 1995 hadi 2016

(i) Kumekuwepo na wimbi la uanzishwaji na upanuzi wa ardhi za hifadhi jambo ambalo limesababisha ongezeko la migogoro ya ardhi hususani katika maeneo ya wafugaji.

(ii) Uwekezaji wa mashamba makubwa ya kilimo cha nishati mimea, miti ya mbao, na mazao ya chakula na biashara umeongezeka. Uwekezaji huu umekwapua ardhi nyingi za vijiji ambazo zilikuwa zikitumiwa na wanavijiji.

(iii) Serikali imeanzisha miradi mikubwa ya kilimo katika ukanda wa Kusini (SAGCOT). Uwekezaji huu utafanyika katika eneo la ukubwa wa theluthi moja ya ardhi yote Tanzania Bara na utaweza kusababisha ongezeko kubwa la migogoro ya watumiaji wa ardhi.

(iv) Viwanda vingi vimefunguliwa, machimbo ya madini yameanzishwa sehemu mbalimbali, na aina mpya za madini na gesi asilia zimegundulika nchini. Sambamba na hayo kumetokea uvunjifu wa haki za binadamu na za ardhi katika maeneo hayo.

(v) Utekelezaji wa miradi hii yote umefanyika kwa kutumia mamlaka za Miliki ya Hatima, na si wakati wote mwenye Uamuzi wa mwisho, yaani Rais, alikuwa na taarifa halisi na athari za uamuzi anaochukua kwa walio wengi – yaani wanavijiji.

### Mapendekezo juu ya Milki ya Hatma

(i) Wanavijiji wenyewe, kupitia vyombo vyao vya kidemokrasia, hususan Mkutano Mkuu wa Kijiji, ndio wawe na miliki ya hatima ya ardhi ya kijiji,

(ii) Kiundwe chombo tofauti cha kitaifa kitakachokuwa na miliki ya hatima ya ardhi isiyo ya vijiji, yaani ardhi ya jumla na ardhi ya hifadhi, ambacho kitawajibika moja kwa moja kwa chombo kikuu cha kitaifa cha uwakilishi, yaani, Bunge.

## 4.5 USAWA WA HAKI ZA ARDHI KIJINSIA

Rasimu ya Sera inasema Serikali itahakikisha:

(i) Kuwepo usawa katika upatikanaji wa ardhi bila ya ubaguzi wowote.

(ii) Wanawake kupata ardhi bila kizuizi chochote kinachosababishwa na mila, desturi, na tamaduni.

(iii) Usawa kati ya wanaume na wanawake katika uwakilishi wa usimamizi wa ardhi.

**Muktadha:** Kwa mara ya kwanza katika Sera suala la jinsia na usawa linatambulika kama suala mtambuka na kupewa uzito wa kipekee. Hata hivyo mbali na kuwa suala hili limepewa sura ya kipekee, halionekani katika sura zote na matamshi yote ya Rasimu.

### Maana ya Sera hii ni;

(i) Usawa katika upatikanaji wa ardhi unatambuliwa na ubaguzi unakataliwa. Lakini sera haibainishi wazi suala hili.

(ii) Usawa katika umiliki na udhibiti. Kiuhalisia, wanawake na wanaume wanayo fursa na haki ya kupata na kutumia ardhi, lakini wanawake huwa hawana haki ya kumiliki na kudhibiti ardhi. Yaani, hawana sauti na maamuzi juu ya ardhi na mazao yatokanayo na ardhi.

(iii) Serikali itakabili vizuizi vya mila, desturi na tamaduni ambavyo humzuia mwanamke kupata ardhi. Hii ni kiini macho tu, kwani zipo sheria mbalimbali ambazo zinatambua matumizi ya mila, desturi na tamaduni katika masuala ya mirathi, ardhi, na usuluhishi wa migogoro. Pia kuna maamuzi ya mahakama za juu zinazoruhusu matumizi ya mila, desturi, na tamaduni. Aidha, sera haitoi jukumu kwa serikali juu ya vizingiti hivyo ambavyo vinazuia umiliki na udhibiti wa ardhi kwa wanawake.

(iv) Usawa wa ushiriki wa wanaume na wanawake katika usimamizi wa ardhi ni jukumu la serikali. Hili ni jambo zuri, lakini uhalisia ni kwamba, wanawake wamekuwa wakihusishwa bila kupewa maamuzi. Hata hivyo, mikutano ya vyombo hivi vya maamuzi vimekuwa vikifanyika muda na nyakati ambazo si rafiki kwa wanawake.

### Uhalisia wa Usawa wa Haki za Ardhi Kijinsia tangu 1995 hadi 2016

(i) Katika Sera na Sheria, hakuna mabadiliko makubwa yaliyotokea katika kipindi hiki. Mbali na kwamba sheria na sera zinatambua usawa na ushiriki wa jinsia zote mbili, uhalisia ni kwamba wanawake wachache sana wamenufaika na haki hizo.

(ii) Bado zipo sheria za mirathi, za kimila na kidini, ambazo ni kandamizi kwa wanawake.

(iii) Kumekuwepo kwa uvunjifu wa haki za wanawake katika ardhi na kutoshirikishwa katika ufanyaji wa maamuzi wakati wa uhawilishaji wa ardhi na katika ulipaji wa fidia.

(iv) Kumekuwa na ongezeko la asasi za kiraia ambazo zinatetea haki za wanawake na kuchochea mabadiliko ya mitazamo na mila na desturi kandamizi.

(v) Uko mwamko mkubwa katika jumuiya ya kimataifa kuhakikisha kuwa haki za wanawake katika ardhi zanatambulika, zinatetewa, na kulindwa.

### Mapendekezo juu ya Usawa wa Haki za Ardhi Kijinsia

(i) Uwekwe utaratibu wa wanawake kumiliki na kudhibiti ardhi. Suala la jinsia liwekwe katika maeneo mengine ya kisera.

(ii) Uwekwe utaratibu wa kidemokrasia wa kuwashirikisha wanawake katika masuala ya utawala wa ardhi.

(iii) Uwekwe utaratibu wa wanawake kushirikishwa na kunufaika na fidia pale ambapo ardhi ya familia inapotwaliwa au kuuzwa.

(iv) Utaratibu wa kisheria pamoja na mila, desturi, na tamaduni zinazolinda haki ya wanawake zitumike katika masuala yote ya ardhi ili kuweza kuepuka matumizi ya mila, desturi, na tamaduni ambazo ni kandamizi kwa wanawake.

## 4.6 UFUATILIAJI NA TATHMINI YA SERA YA ARDHI

Rasimu ya Sera inasema kutaanzishwa mfumo wa ufuatiliaji na tathmini wa Sera ya taifa ya ardhi.

**Muktadha:** Hili ni jambo jipya linaloletwa na Rasimu ya Sera ya Taifa ya Ardhi 2016. Ufuatiliaji na tathmini utasaidia kuhakikisha mipango yote ya utekelezaji wa Sera inafuatiliwa na kutathminiwa na wadau mbalimbali kila mwaka.

### Maana ya Sera hii ni;

(i) Dola kupitia Wizara ya Ardhi itaunda mfumo wa kielektroniki ambao utasaidia kukusanya, kuchambua, na kusambaza taarifa mbalimbali zihusuzo utekelezaji wa Sera kila mwaka.

(ii) Wadau mbalimbali kuanzia ngazi ya kijiji hadi taifa watashirikishwa katika mchakato mzima wa ufuatiliaji na tathmini ya Sera.

(iii) Takwimu za masuala ya ardhi, kisera na utekelezaji, zitakuwa zikipatikana kwa urahisi zaidi.

(iv) Japo haya yanaonekana ni mazuri, Wizara ya Ardhi bado haijatoa mpango mkakati wa utekelezaji wa Sera. Mpango ambao ndio msingi wa ufuatiliaji na tathmini.



### Uhalisia juu ya Ufuatiliaji na Tathmini ya Sera ya Taifa ya Ardhi tangu 1995-2016

(i) Ni vigumu kupata taarifa ya uhakika, sahihi na ya wakati katika masuala ya ardhi,

(ii) Wizara imetekeleza mpango mkakati wa utekelezaji wa sheria za ardhi wa mwaka 2005 bila mafanikio kwa sababu mbalimbali ikiwemo uhaba wa fedha. Mwaka 2013 Wizara iliandaa mpango mkakati wa pili wa utekelezaji wa sheria za ardhi. Hadi sasa hakuna taarifa rasmi inayo onyesha namna mikakati hii imetekelezwa na mafanikio yake,

(iii) Kwa miaka ya karibuni, Wizara imekuwa ikifanya jitihada za kuboresha mfumo wa upatikanaji, utunzaji na usambazaji wa taarifa za ardhi,

(iv) Katika ngazi ya kimataifa, jumuiya ya kimataifa imepitisha malengo ya maendeleo endelevu 2030 ambayo kwa mara ya kwanza inaweka malengo katika masuala ya ardhi. Nchi zote zitatakiwa kutoa taarifa za masuala ya ardhi. Hivyo basi, Tanzania inajukumu la kuhakikisha mfumo wa ufuatiliaji na tathmini unakuwepo na unatekelezwa.

### Mapendekezo juu ya Ufuatiliaji na Tathmini ya Sera ya Taifa ya Ardhi

(i) Katika ngazi ya kijiji, iwepo agenda ya kudumu ya masuala ya ardhi katika Mikutano Mikuu na mikutano ya Halmashauri ya Kijiji. Taarifa za masuala ya ardhi za kila kijiji ziwasilishwe wilayani na nakala zake ziwepo katika ngazi ya kata kila baada ya mkutano mkuu kufanyika,

(ii) Katika ngazi ya Taifa, uwepo mkutano wa kitaifa wa wadau ambao utawezesha wadau kujadili vipaumbele na bajeti, taarifa ya utekelezaji, na taarifa za ufuatiliaji na tathmini kila mwaka. Mchakato huu usihodhiwe na Serikali bali ushirikishe wadau wengine kama vile asasi za kiraia na taasisi za utafiti wapewe fursa ya kuwasilisha taarifa zao,

(iii) Serikali itenge bajeti kutokana na vyanzo vyake vya ndani ili kuhakikisha kuwa mipango ya ufuatiliaji na tathmini ya utekelezaji wa Sera ya Ardhi unatekelezeka bila kuathiriwa na siasa au mabadiliko yatokanayo na utegemezi wa fedha za wahisani.




# SURA YA TANO

## 5.0 HITIMISHO

Ni muhimu kufahamu kuwa Sera ya Taifa ya Ardhi ni dira na mwongozo kuhusiana na masuala yanayohusu rasilimali ardhi. Marekebisho ya Sera yatakapokamilika ndiyo yatakayotoa mwelekeo wa marekebisho ya Sheria za Ardhi zilizopo, mfano Sheria ya Ardhi Namba 4 ya mwaka 1999, Sheria ya Ardhi ya Vijiji Namba 5 ya mwaka 1999, Sheria ya Utatuzi wa Migogoro ya Ardhi Namba 2 ya mwaka 2002 na Sheria nyinginezo. Kwa maana hiyo ni muhimu kwa wananchi hasa wazalishaji wadogowadogo ambao ndio watumiaji wakubwa wa ardhi katika uzalishaji mali kuhakikisha kuwa wanapata fursa ya kutoa maoni yao kuhusu rasimu ya Sera hii. Chapisho hili linachambua maeneo makuu ya Sera kuhusu upatikanaji, matumizi, umiliki wa ardhi na utatuzi wa migogoro ya ardhi nchini. Kwa kutumia chapisho hili wadau mbalimbali wa masuala ya ardhi wataweza kuishawishi serikali kuzingatia maoni ya muda mrefu ya wananchi kuhusu mfumo wa milki ya ardhi wenye kulinda maslahi ya watumiaji ardhi hasa wazalishaji wadogowadogo.

# NOTE




**KWA MAWASILIANO ZAIDI TUMIA ANUANI ZIFUATAZO**

**TANZANIA LAND ALLIANCE (TALA)**

**Simu: +255689338721, Barua pepe: tanzanialandalliance@gmail.com**


ROSA LUXEMBURG STIFTUNG HAMBURG


Kijarida hiki kimechapishwa kwa hisani ya Rosa Luxemburg Foundation (RLS inafadhiliwa na Wizara ya ushirikiano wa kiuchumi na maendeleo ya Ujerumani)